# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA MHESHIMIWA CHARLES N. KEENJA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA 2001/2002

## I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali inayohusu Wizara ya Kilimo na Chakula na baada ya kuzingatia taarifa hiyo, naomba kutoa hoja, kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa mwaka wa fedha wa 2001/2002.

2. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza ya Bajeti baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Benjamin William Mkapa kwa kuchaguliwa kwa kura nyingi kuendelea kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, Mbunge wa Hanang, kwa kuteuliwa tena kuwa Waziri Mkuu.

3. Aidha, tunakupongeza wewe, Mheshimiwa Pius Msekwa, kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Bunge, Mheshimiwa Juma Jamaldin Akukweti, Mbunge wa Tunduru, kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika na Waheshimiwa Anna Makinda, Mbunge wa Njombe Kusini na Eliachim Simpasa, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge. Tunawahakikishia ushirikiano.

4. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Chakula, Washikadau wa Sekta ya Kilimo, wananchi wa Jimbo la Ubungo ninaowawakilisha hapa Bungeni na kwa niaba yangu mwenyewe, tunaungana na Watanzania wenzetu kumpa pole Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, kwa kifo cha ghafla cha aliyekuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Dkt. Omar Ali Juma. Ninatoa salamu za rambirambi kwa mjane, familia yote ya marehemu na kwa Taifa kwa jumla.

5. Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wizara ya Kilimo na Chakula na kwa niaba ya washikadau wote wa Sekta ya Kilimo, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninamhakikishia ushirikiano wa dhati wa Wizara ya Kilimo na Chakula.

6. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi tisa tangu Uchaguzi Mkuu wa mwaka wa 2000, tumewapoteza Waheshimiwa Wabunge wenzetu wanne: Marehemu Ernest Nyanda, aliyekuwa Mbunge wa Busega; Marehemu Profesa Crispin Donald Hauli, aliyekuwa Mbunge wa Ludewa; Marehemu Bhiku Mohamed Bhiku, aliyekuwa Mbunge wa Solwa na Marehemu Abbas Gulamali, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero.Wapo pia Madiwani waliofariki katika kipindi hiki. Mungu alaze roho zao mahali pema peponi na aziimarishe familia zao.

7. Mheshimiwa Spika, mwaka huu, Serikali na viongozi wetu wa ngazi ya juu wameweka msukumo mpya katika Sekta ya Kilimo. Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, aliitisha na kuendesha mkutano wa washikadau wa Sekta ya Kilimo kwa siku mbili, tarehe 23 na 24 Machi, 2001 hapa Dodoma. Makamu wa Rais, hayati Dkt. Omar Ali Juma, aliendesha mkutano wa washikadau wa Pamba tarehe 17 na 18 Aprili, 2001 mjini Mwanza na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Tluway Sumaye, (Mb.) aliendesha mkutano wa washikadau wa Sekta ya Kahawa tarehe 12 na 13 Mei, 2001 mjini Moshi. Mikutano hii ilipendekeza hatua za kuchukua ili kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo. Aidha Serikali, imekuwa ikichukua hatua za kuweka mazingira ya kukifanya kilimo kiwavutie wawekezaji. Hatua hizo ni pamoja na kuondoa kabisa au kupunguza kodi za mazao na mahitaji yote ya kilimo, kuyatoza kodi mazao yanayotoka nje ili kuondoa ushindani na yale yanayozalishwa nchini na kurekebisha

sheria ili kuondoa vipengele vilivyokuwa na utata.

8. Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri walionitangulia ambao hotuba zao zimegusia na kufafanua masuala mengi yanayohusu kilimo. Shukrani na pongezi pia ziwaendee Waheshimiwa Wabunge kutokana na michango yao wakati wa kujadili hotuba hizo. Michango yenu imeonyesha hamasa ya kutaka sekta ya kilimo iongezewe raslimali ili ikue, izalishe chakula cha kutosha na kuwaondolea wananchi umaskini.

9. Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa wabunge walioteuliwa kuwa wajumbe wa Kamati hiyo. Kamati hiyo ilichambua kwa umakini na ustadi taarifa na makadirio ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Nawashukuru wanakamati kwa maoni, mapendekezo na maelekezo waliyotoa na nawahakikishia kwamba kadri itakavyowezekana, yatazingatiwa na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake.

## II. HALI YA KILIMO NCHINI

10. Mheshimiwa Spika, sekta ya kilimo inachangia wastani wa asilimia 50 ya pato la Taifa na zaidi ya asilimia 60 ya mapato ya fedha za kigeni kwa mwaka. Sekta ndogo ya mazao inachangia asilimia 35 ya pato la Taifa na sehemu iliyobaki inachangiwa na sekta ndogo za mifugo, uvuvi na misitu. Kilimo kinaajiri karibu asilimia 80 ya nguvukazi. Aidha, kilimo ndicho kinachotoa mitaji ya kujenga viwanda na mali ghafi zinazotumika kwenye viwanda hivyo.

11. Mheshimiwa Spika, kilimo kinawapatia Watanzania wanaokisiwa kuwa milioni 30, mahitaji yao ya chakula. Inakisiwa kwamba kati ya asilimia 95 na 97 ya chakula chetu kinazalishwa humu nchini na asilimia 3 hadi 5 tu ndiyo inayoagizwa kutoka nje ya nchi. Hali hii inaleta matumaini. Hata hivyo inakisiwa kwamba karibu asilimia 40 ya familia za Kitanzania hazipati chakula cha kutosha au chenye ubora unaotakiwa, ama kutokana na familia hizo kutozalisha chakula cha kutosha au kutokuwa na uwezo wa kujinunulia chakula cha kutosha.

12. Mheshimiwa Spika, kilimo cha Tanzania kinategemea wakulima wadogo, hususan wanawake na wazee, ambao mapato yao ni madogo, ujuzi wao wa kilimo cha kisasa ni mdogo na zana wanazotumia ni duni na zinazotegemea nguvu za mwanadamu. Mashamba yao ni madogo yenye ukubwa wa hekta 0.5 hadi 3.0.

13. Kilimo chetu kinakabiliwa na matatizo mengi yanayosababisha kushuka kwa uzalishaji na mapato. Matatizo hayo ni pamoja na:-

- Kuvurugika kwa utaratibu wa kuagiza na kusambaza pembejeo za kilimo;
- uwekezaji mdogo;
- matumizi madogo ya zana zinazorahisisha kazi;
- gharama kubwa za umeme zinazofanya kilimo cha umwagiliaji na viwanda vya kusindika mazao visiweze kuendeshwa kwa faida;
- kukosekana kwa masoko ya uhakika kwa mazao yetu makuu;
- kushuka sana kwa bei za mazao makuu ya biashara;
- kutokuwapo kwa taasisi imara za wakulima;
- janga la UKIMWI linalotupunguzia nguvukazi;
- miundombinu mibovu sana; na
- uharibifu wa mazingira.

**Uwezo wa Uzalishaji katika Kilimo**

14. Nchi yetu ina hekta 43 milioni zinazofaa kwa kilimo. Tunalima hekta milioni saba tu, au asilimia 16 ya eneo linalofaa kwa kilimo. Inakisiwa kwamba kuna hekta karibu milioni moja zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji maji mashambani. Tunamwagilia hekta 160,000 tu sawa na asilimia 16 ya eneo linalofaa kwa umwagiliaji. Tuna nguvukazi ya kutosha na tuna ujuzi wa kutuwezesha kuongeza uzalishaji wa kilimo. Changamoto tulilonalo **ni kuondoa matatizo yaliyopo ili yaruhusu kutafsiriwa kwa uwezo uliopo katika uzalishaji halisi.**

**Ukuaji wa Sekta ya Kilimo 1998 – 2001.**

15. Mheshimiwa Spika, wastani wa ukuaji wa sekta ya kilimo kwa miaka mitatu iliyopita ulikuwa asilimia 3.3. Katika mwaka wa 1998 sekta ya kilimo ilikua kwa kiwango cha asilimia 1.9, mwaka wa 1999 asilimia 4.1 na mwaka wa 2000 kwa na asilimia 3.7. Ukuaji huu mdogo wa uzalishaji katika sekta ya kilimo ulisababishwa kwa kiasi kikubwa na hali mbaya ya hewa, milipuko ya magonjwa, wadudu na wanyama waharibifu wa mimea na mazao na matumizi madogo ya pembejeo. Katika mwaka wa 2001, sekta ya kilimo inatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimi 4.3.

**Mazao ya Chakula**

16. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001, mahitaji ya chakula humu nchini yalikuwa jumla ya tani milioni 7.88 wakati uzalishaji ulikuwa tani milioni 7.31. Hivyo, kulikuwapo upungufu wa tani 565,000 kutokana na ukame uliojitokeza katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Iringa, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Mara, Tabora na Singida. Katika mwaka wa 2000/2001, mvua za vuli na masika zilikuwa za kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi, hivyo, upatikanaji wa chakula katika mwaka wa 2001/2002 utakuwa mzuri. Hata hivyo, mvua katika mikoa ya Kagera, Mwanza, Mara, Shinyanga, Arusha na Kilimanjaro zilinyesha kwa mtawanyiko mbaya na katika baadhi ya maeneo zilinyesha chini ya wastani. Mahitaji ya chakula kwa mwaka wa 2001/2002 yanakadiriwa kuwa tani milioni 8.13 na uzalishaji tani milioni 7.712 na hivyo kuashiria upungufu wa tani 419,000 za chakula.

17. Mheshimiwa Spika, wananchi wanashauriwa kujiwekea akiba ya chakula cha kutosha hadi msimu ujao. Biashara ndani ya nchi iwe huru na kusiwepo vizuizi vyovyote vya kuhamisha chakula kutoka eneo moja la nchi kwenda eneo jingine. Mkoa wa Rukwa umeruhusiwa kuuza chakula kwenye nchi zinazopakana na Mkoa huo na uwezekano wa kuiruhusu mikoa mingine yenye matatizo sawa na yale ya Mkoa wa Rukwa kuuza chakula nje ya mipaka yetu unatazamwa.

18. Hali ya chakula katika nchi zinazotuzunguka nayo si ya kuridhisha. Uzalishaji wa mahindi katika nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia na Zimbabwe unatarajiwa kupungua kwa asilimia 27 ukilinganishwa na mwaka wa 2000/2001 kutokana na mafuriko yaliyoathiri watu wanaokisiwa kufikia 900,000. Aidha upatikanaji wa Chakula katika nchi za Kongo, Rwanda na Burundi si wa kuridhisha kutokana na vurugu za kisiasa na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

**Mazao ya Biashara**

19. Mheshimiwa Spika, ukuaji wa uzalishaji wa mazao ya biashara kati ya mwaka wa 1995 na mwaka wa 2001 ulikuwa wastani wa asilimia 5.4. Hali ya uzalishaji wa mazao makuu ya biashara katika mwaka wa 2000/2001 ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na.1: Uzalishaji wa Mazao ya Biashara 1999/2000 na 2000/2001**

| **Aina ya Zao** | **1999/2000 (Tani)** | **2000/2001 (Tani)** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Kahawa | 47,811 | 57,988 | 21.3 |
| Pamba | 196,000∗ | 228,591∗ | 16.7 |
| Korosho | 121,200 | 127,900 | 5.5 |
| Tumbaku | 25,432 | 24,247 | -4.7 |
| Chai | 23,600 | 25,500 | 8.1 |
| Mkonge | 20,600 | 20,500 | -0.5 |
| Pareto | 738 | 1,750 | 137.0 |
| Sukari | 116,933 | 134,000 | 15.1 |
| MazaoYasio Asili | 540,124 | 407,127 | -24.6 |

*Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula ∗ = Marobota*

Uzalishaji wa mazao ya biashara katika mwaka wa 1986/87-2000/2001 unaonyeshwa katika Kiambatanisho Na.3.

## III: UTEKELEZAJI WA KAZI KWA MWAKA WA 2000/2001

### Utafiti wa Mazao ya Kilimo

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 utafiti wa kilimo uliendelea katika vituo vyote 17 vya Wizara kwa lengo la kumpatia mkulima tekinolojia bora zaidi za kumwezesha kuzalisha kwa gharama nafuu, na hivyo kumwongezea tija na faida na hatimaye kumpunguzia umasikini. Taasisi mbili zinazojitegemea za kusimamia utafiti wa zao la kahawa "*Tanzania Coffee Reseach Institute - TACRI*" na zao la tumbaku "*Tobacco Research Institute of Tanzania – TORITA*" zimesajiliwa. Aidha, vituo vya utafiti vilitoa aina bora za mbegu za mazao kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na.2: Mbegu bora ambazo utafiti wake umekamilika msimu wa 2000/2001**

| KITUO | ZAO | SIFA |
|---|---|---|
| **UKIRIGURU**<br><br><br><br>**UYOLE** | <u>**Viazi Vitamu:**</u><br>§ Mbegu bora aina 4 **Juhudi, Vumilia, Sinia** na **Simama**<br><u>**Mahindi:**</u><br>§ Aina 3 za mbegu chotara | § Uwezo wa kuzaa **tani 15** za viazi badala ya **tani 6** kwa mbegu zilizopo. Tayari mbegu zinasambazwa.<br>§ Uwezo wa kuzaa **tani 6-8** kwa hekta, na **kustahimili ugonjwa hatari wa ukungu wa mahindi – "Grey Leaf Spot" –** Tani 120 za mbegu zitatolewa msimu wa 2001/2002 |
| **SELIAN** | § <u>**Mahindi:**</u><br>Aina 2 za mbegu bora | § Uwezo mkubwa wa **kustahimili ukame,** na **kukua kwenye ardhi yenye upungufu wa virutubisho** (Low Nitrogen Drought Tolerant maize). Production:<br><br>§ **Lishe bora** (Quality Protein Maize – QPM) ili **kukabiliana na utapiamlo.** |

| | | |
|---|---|---|
| **KATRIN Ifakara** | **<u>Mpunga:</u>**<br>Aina mbili za mbegu bora Line 85 na Line 88 | § **Ladha nzuri na mavuno mengi (tani 6-8 kwa hekta).** Mbegu ya msingi inazalishwa. |

| | | |
|---|---|---|
| **ILONGA** | -<br>**<u>Mbaazi</u>**<br><br>**<u>Kunde</u>**<br><br>-<br>**<u>Pamba</u>**<br>- aina ya IL 90<br><br>-<br>-<br>**<u>Mtama</u>** aina tatu za mbegu bora | § **Zinakomaa katika siku 90-120** badala ya simu 130-270.<br><br>§ **Zinakomaa katika siku 60** badala ya siku 90-110,<br><br>§ Hutoa tani 1.5 kwa hekta badala ya tani 0.4-0.6 kwa hekta.<br><br>§ Ina **nyuzi nyingi** zaidi **asilimia 36-38** badala ya asilimia 33-35.<br><br>§ **Ngumu**<br><br>§ Zina **ukinzani mkubwa** (resistance) dhidi ya **gugu la kiduha (striga)** |

**Huduma za Ugani**

21. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 shughuli za huduma za ugani ziliendelea kutolewa na maafisa ugani ambao tangu mwaka wa 1998 wanasimamiwa na Serikali za Mitaa. Wizara inaendelea kutoa vitendea kazi *(Kiambatisho Na.4)*, ushauri wa kitaalam na miongozo ya utekelezaji wa shughuli za kilimo kwa watumishi hao. Vile vile, Wizara iliagiza magari 50 na pikipiki 1,200 ambazo zitagawiwa zitakapowasili. Serikali za Mitaa zinatakiwa kuwatumia maafisa kilimo kikamilifu na kuwawezesha kufanya kazi zao kwa ufanisi.

**Udhibiti wa Magonjwa na Visumbufu vya Mimea na Mazao.**

22. Mheshimiwa Spika, Wizara, kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, na mashirika yasiyo ya kiserikali, ilidhibiti visumbufu vya mimea na mazao kwenye mikoa iliyovamiwa, kwa kutumia mbinu za udhibiti husishi *(Integrated Pest Management)*, udhibiti kibiolojia na matumizi ya madawa. Visumbufu hivyo ni kama vifuatavyo:-

- Milipuko ya **panya** iliikumba mikoa ya **Lindi, Morogoro, Mbeya** na **Tanga;**

- *Quelea quelea* walivamia mikoa ya **Dodoma, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Singida na Tabora;**

- **Nzige** walienea kwenye eneo la zaidi ya **kilometa 43** za mraba katika mbuga za **Iku – Katavi mkoani**

**Rukwa;**

- **Viwavijeshi walivamia** jumla ya **hekta 7,800** za **mashamba** ya mahindi, mtama, uwele, na malisho ya mifugo katika mikoa ya **Dodoma, Morogoro, Arusha, Iringa, Ruvuma** na **Singida;**

- **Kidung'ata** wa muhogo waliendelea kushambulia zao la muhogo katika mikoa ya **Pwani, Dar es Salaam, Ruvuma, Iringa, Mbeya, Mtwara, Mara, Mwanza** na **Morogoro;**

- Kadhalika, zao la **muhogo** lilishambuliwa na ugonjwa wa **batobato** *(Cassava Mossaic Disease)* katika mikoa ya **Kagera** na **Mwanza**.  Ugonjwa huu unaenea kwa kilomita 70 kwa mwaka.

Katika mwaka wa 2001/2002 udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao utaendelea kuimarishwa na Wizara itajenga uwezo wa kudhibiti milipuko ya visumbufu bila kuchelewa.

**Upotevu wa Mazao**

23. Mheshimiwa Spika, upotevu wa mazao baada ya kuvunwa unakisiwa kuwa kati ya asilimia 30 na 40 kwa mwaka. Miongoni mwa visumbufu vinavyosababisha upotevu mkubwa hasa kwenye nafaka ni panya, mchwa, wadudu jamii ya nondo na jamii ya mbawakavu, hususan dumuzi. Wizara iliendelea kushirikiana na Serikali za Mitaa na baadhi ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kutoa **mafunzo kwa maafisa ugani na wakulima** juu ya njia bora za kuhifadhi mazao. Halikadhalika, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Ushirikiano wa Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)* iliendeleza udhibiti wa visumbufu wa mazao kibiolojia na kwa kutumia madawa ya asili katika mikoa ya **Morogoro, Dodoma, Iringa, Arusha, Kilimanjaro** na **Shinyanga.** Aidha, **tafiti** mbalimbali juu ya teknolojia za kupunguza upotevu wa mazao zinaendelea katika vituo vyetu vya utafiti vya Uyole, Tengeru, TPRI na katika kituo cha udhibiti wa panya kilichoko Morogoro.

**Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani**

24. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 Wizara ya Kilimo na Chakula iliendelea kutilia mkazo kilimo cha umwagiliaji maji. Miradi saba ya umwagiliaji maji ya wakulima wadogo ilijengwa au kukarabatiwa. Miradi hiyo ina jumla ya hekta 14,667 na imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji. Itakapokamilika inatarajiwa kuongeza uzalishaji wa mpunga kwa tani 58,668.  Wilaya 18 zitafaidika kama ifuatavyo:-

- Mradi wa Usimamizi wa Mabonde ya Mito Rufiji na Pangani na Uboreshaji wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Maji Mashambani kwa Wakulima Wadogo (*Rufiji and Pangani River Basins Management and Smallholder Irrigation Improvement Project*), **unaotekelezwa katika Wilaya za Korogwe, Arumeru, Moshi, Simanjiro, Iringa Vijijini na Mbarali.**

- Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support- ASPS*), **unaotekelezwa kwenye wilaya za Kilosa, Iringa Vijijini, Mbeya Vijijini na Mbozi.**

- Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*Participatory Irrigation Development Programme-PIDP*), **unaotekelezwa kwenye wilaya za Dodoma Vijijini, Manyoni, Nzega, Shinyanga Vijijini, Kwimba na Babati.**

- Miradi ya Kilimo cha Umwagiliaji ya **Mwega (Kilosa), Madibira (Mbarali) na Kitivo (Lushoto).**

## Upatikanaji wa Pembejeo na Zana za Kilimo

25. Mheshimiwa Spika, matumizi ya pembejeo za kilimo nchini ni madogo sana kutokana na kuvurugika kwa mfumo wa upatikanaji na usambazaji wa pembejeo nchini, hasa baada ya kuanzishwa kwa sera ya soko huru na kuondolewa kwa ruzuku ya mbolea kuanzia mwaka wa 1992. Aidha, matumizi ya pembejeo ni madogo kutokana na wakulima wengi kutokuwa na uwezo wa kuzinunua na kutokuwepo utaratibu wa kuwapatia mikopo na kupanda sana kwa bei za pembejeo.

26. Kama **hekta milioni saba zinazolimwa** nchini zingewekewa kiasi cha mbolea kinachotakiwa, mahitaji ya mbolea nchini yangekuwa zaidi ya tani 400,000 kwa mwaka. Mwaka wa 2000/2001 makadirio ya mahitaji ya pembejeo yaliyowasilishwa na mikoa na upatikanaji ulikuwa kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na.3: Makadirio ya Mahitaji na Upatikanaji wa Pembejeo katika Mwaka wa 2000/2001**

| Aina ya Pembejeo | Mahitaji | Upatikanaji | Asili-Mia | Ziada/Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| | | Kiasi | | |
| Mbolea | tani 170,000 | tani 112,000 | 66.0 | tani (68,000) |
| Mbegu | tani 38,000 | tani 8,196 | 21.6 | tani (29,804) |
| Madawa | lita 3,200,000 | lita 3 ,000,000 | 93.7 | lita (200,000) |
| Madawa (unga) | tani 9,000 | tani 6,000 | 66.7 | tani (3,000) |

*Chanzo:* *Wizara ya Kilimo na Chakula*

Aidha, tani 2,934 za mbegu za aina mbalimbali za msaada kutoka kwa wahisani kwa ajili ya wananchi walioathirika na ukame zilisambazwa.

## Mfuko wa Pembejeo

27. Mheshimiwa Spika, **Serikali imeamua kwamba mfuko huo utaendelea kuwapo.** Katika mwaka 2000/2001, Mfuko wa Pembejeo za Kilimo haukukopesha kutokana na Mfuko kutokusanya madeni ya mikopo. Hadi mwaka wa 2000, Mfuko ulikuwa umetoa mikopo 259 kwa mawakala wa pembejeo na wakulima yenye thamani ya shilingi bilioni 5.8. Kati ya hizo, shilingi bilioni 2.03 zilikuwa zimerejeshwa kufikia Juni 2001. Hatua za kuwahimiza wadaiwa kurejesha mikopo yao zimechukuliwa, ikiwa ni pamoja na kuwasiliana nao na kuwachukulia hatua za kisheria. Matokeo ya hatua zilizochukuliwa yanatia moyo kwani baadhi ya wadaiwa wameanza kulipa mikopo yao. Kuanzia mwaka wa 2001/2002 fedha za Mfuko zitapitishwa kwenye Benki kwa utaratibu utakaowekwa.

28. Mheshimiwa Spika, matumizi ya zana za kurahisisha kazi katika kilimo bado ni madogo. Inakadiriwa kuwa yapo matrekta 8,414 yanayofanya kazi na 6000 ambayo ni mabovu yanayotengenezeka. Eneo linalolimwa kwa matrekta ni asilimia 10, wanyamakazi asilimia 20 na jembe la mkono asilimia 70. Katika kukabiliana na tatizo la upatikanaji wa zana bora za kilimo, Wizara, kupitia kwa wahisani, hususan Serikali za Japan na Korea, iliingiza nchini matrekta madogo ya mkono *(power tillers)* 32 katika mwaka 2000 na 170 mwaka 2001. Katika mwaka wa 2001/2002 Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuagiza matrekta mapya na yaliyotumika yenye bei nafuu na kuanzisha vituo vya kukodishia zana za kilimo na kuuza pembejeo. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya

Viwanda na Biashara, itahimiza kufufuliwa kwa viwanda vya zana za kilimo KIZAKU (Mbeya) na UFI (Dar es Salaam).

**Ubinafsishaji wa Mashirika ya Kilimo**

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 mashirika ambayo yamebinafsishwa ni Makao Makuu ya Shirika la Usagishaji la Taifa *(NMC)* na Mamlaka ya Chai matawi ya Dabaga, Iringa; Maruku, Bukoba; Mponde, Tanga na Rungwe, Mbeya. Mkakati wa ubinafsishaji wa mashamba makubwa ya NAFCO meandaliwa. Aidha, ubinafsishaji wa viwanda vya korosho unaandaliwa kwa kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na unakaribia kukamilika. Katika mwaka wa 2001/2002 ubinafsishaji wa mashirika haya utakamilishwa. Aidha, Kampuni ya mbegu TANSEED, kiwanda cha Chai Lupembe, Njombe na kampuni ya sukari Kagera vitabinafsishwa.

**Maendeleo ya Watumishi**

30. Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo hawakupandishwa vyeo kwa utaratibu uliowekwa na Serikali. Ili kuwaondolea watumishi kero hii, kibali cha kuwapandisha vyeo watumishi **6,865** kilitolewa na Idara Kuu ya Utumishi mwaka wa 2000/2001. Tume ya Utumishi Serikalini imekwisha kuwapandisha vyeo viwili viwili watumishi **1,528** wa kada na madaraja mbalimbali. Wote wamekwisha kupelekewa barua zao za kupandishwa vyeo.

31. Katika mwaka wa 2001/2002 Wizara itaendelea kufuatilia upandishwaji vyeo watumishi **5,337** waliobaki na itashughulikia kuwabadilishia vyeo watumishi ambao wamejiendeleza kitaaluma na kupata sifa za nyongeza. Aidha, kumbukumbu zote za wafanyakazi zitahifadhiwa kwenye kompyuta ili iwe rahisi kuzifanyia rejea kila mwaka. Kwa watumishi walio chini ya Serikali za Mitaa, Halmashauri husika zitarekebisha mishahara yao baada ya kupokea barua za kupandishwa vyeo watumishi wake. **Napenda kuwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Kilimo na Chakula kwa uvumilivu mkubwa walioonyesha katika mazingira magumu bila ya kupandishwa vyeo.**

**Matumizi ya Fedha za Bajeti ya Mpango wa Mwaka wa 2000/2001**

32. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2000/2001 Wizara ilikadiriwa kutumia Jumla ya shilingi 32,038,404,300/= kama ifuatavyo:-

| **MAKADIRIO** | **Shilingi** |
|---|---|
| Matumizi ya kawaida | 10,163,404,300/= |
| Matumizi ya miradi ya maendeleo | 21,875,000,000/= |
| *Fedha za hapa* | *2,271,000,000/=* |
| *Fedha za Nje* | *19,604,000,000/=* |
| **JUMLA** | **32,038,404,300/=** |

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2001, matumizi ya fedha yalikuwa ni jumla ya shilingi 23,320,562,560/= kama ifuatavyo:-

| **MATUMIZI** | **Shilingi** |
|---|---|
| Matumizi ya kawaida | 10,314,322,922/=. |
| Matumizi ya miradi ya maendeleo | 13,006,239,638/= |

| | |
|---|---|
| *Fedha za hapa* | *1,989,153,000/=* |
| *Fedha za Nje* | *11,017,086,638/=* |
| **JUMLA** | **23,320,562,560/=** |

Matumizi ya fedha za kawaida yalikuwa zaidi ya kiasi kilichoidhinishwa kutokana na fedha za ziada *(shilingi 150,918,622/=)* zilizotolewa kwenye Kitengo cha Hifadhi ya Chakula kwa ajili ya kununua chakula kwa walioathirika na njaa.

## IV: KAZI ZITAKAZOFANYIKA MWAKA WA 2001/2002

33. Mheshimiwa Spika, mwezi wa Novemba mwaka wa 2000 iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Ushirika iligawanywa katika Wizara tatu mpya. Wizara hizo ni Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, Wizara ya Ushirika na Masoko na Wizara ya Kilimo na Chakula. Kila Wizara ilipewa majukumu ya msingi. Majukumu ya Wizara ya Kilimo na Chakula ni pamoja na kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera za Kilimo, kuendeleza na kuimarisha huduma za ugani na utafiti, kuendeleza rasilimali ya wafanyakazi na washikadau wa sekta, ujenzi wa maghala ya hifadhi ya chakula, kusimamia matumizi bora ya ardhi ya kilimo, kusimamia usindikaji wa mazao na kusimamia miradi, mashirika, makampuni na mawakala walio chini ya Wizara.

34. Mheshimiwa Spika, mwaka wa 2001/2002 ni mwaka wa kwanza wa kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Tatu ya Chama Cha Mapinduzi. Hivyo, katika kipindi hiki, utekelezaji wa mikakati ya kilimo utazingatia malengo makuu ya kilimo yaliyoainishwa katika Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka wa 2000. Malengo hayo ni:-

- kuwawezesha wakulima kuongeza tija katika uzalishaji wa mazao kwa kila eka kulingana na viwango vya kisasa kwa kila zao linalohusika;
- kuwawezesha wakulima kuongeza maeneo wanayolima; na
- kuwakaribisha na kuwavutia wakulima wa kati na wakubwa wakiwemo wataalamu wa kilimo.

35. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 Wizara ya Kilimo na Chakula itaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuinua kilimo nchini. Wizara itaweka mkazo katika **kuandaa programu za kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo, kutekeleza mradi wa Kuongeza Rutuba kwenye Udongo na Tija katika Kilimo** (*Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project - SOFRAIP*) na **kuandaa Mpango Kabambe wa Umwagiliaji maji Mashambani.** Kazi nyingine zitakazofanywa na Wizara kwa kushirikiana na washikadau wa Sekta zimefafanuliwa kama ifuatavyo:

### Mkakati wa Maendeleo ya Kilimo

36. Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kushirikiana na Wizara za Maji na Maendeleo ya Mifugo, Ushirika na Masoko na washikadau, imeandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo. Dira ya mkakati huu ni kuwa ifikapo mwaka wa 2025, kilimo chetu kiwe cha kisasa, cha kibiashara, chenye tija na chenye faida; kinachohakikisha matumizi endelevu ya maliasili zilizopo na chenye kushirikisha sekta nyingine. Kazi inayofuata ni kuandaa programu za utekelezaji wa Mkakati huo. Programu hizi zitaainisha kwa kina miradi mbalimbali itakayotekelezwa, watakaoitekeleza na gharama za utekelezaji. Wahisani wameonyesha nia ya kuchangia gharama za utekelezaji. Mkakati huu umeandaliwa sambamba na Mkakati wa Maendeleo Vijijini. **Waheshimiwa**

**Wabunge watagawiwa nakala za rasimu ya Mkakati.**

37. Mheshimiwa Spika, katika mkutano wa washikadau wa sekta ya kilimo uliofanyika Dodoma tarehe 23 na 24 Machi 2001, Mheshimiwa Rais aliagiza kila ngazi, kuanzia kijiji, kata, wilaya, mkoa hadi Taifa, kuandaa malengo yake ya kilimo. Aidha, Bodi za Mazao nazo zimetakiwa kuandaa au kurekebisha mikakati yao ya kuendeleza mazao wanayosimamia. Baada ya kukamilika kwa malengo na mikakati ya Mikoa na Bodi za Mazao, programu za utekelezaji zitaandaliwa. Mikoa inahimizwa kukamilisha maandalizi ya mikakati yao na kuiwasilisha Wizarani ili programu za kuitekeleza zijumuishwe katika programu ya Taifa.

**Kuwezesha Wakulima Wadogo na wa Kati Kuongeza Uzalishaji**

38. Mheshimiwa Spika, ili kuwahakikishia wakulima bei nzuri za mazao, Wizara itachukua hatua za kuhakikisha kwamba mazao yanayozalishwa ni ya ubora wa hali juu, na pia kuhimiza kilimo cha mazao yasiyo asilia yenye masoko yenye bei nzuri na ushindani mdogo nje ya nchi yakiwamo viungo, maua, mlonge, kao, soya, mbaazi, maharagwe, mbegu za mafuta na karanga miti *(macademia nuts).*

**Miliki ya Mashamba**

39. Mheshimiwa Spika, tumeendelea kuwa na watu wanaohodhi maeneo makubwa ya ardhi kwenye maeneo yenye miundo mbinu bila kuyalima. Kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi na Mikoa, tunachukua hatua za kubaini mashamba ya aina hiyo na iwapo hayataendelezwa hadi Desemba 2001, hatua za kutengua hati miliki zitachukuliwa ili yatolewe kwa wawekezaji au kwa wananchi watakaoyalima.

**Usindikaji wa Mazao**

40. Mheshimiwa Spika, lengo la Wizara ya Kilimo na Chakula ni kuhakikisha kwamba kadri itakavyowezekana mazao yanayozalishwa humu nchini yanasindikwa kabla ya kuuzwa. Kwa mazao ya chakula, tunao uwezo mkubwa wa kusindika mahindi, ngano na mpunga. Mipango inafanywa ya kupata mwekezaji atakayejenga kiwanda cha kusaga mahindi mjini Sumbawanga kwa lengo la kuuza sembe nchi za jirani. Aidha, kwa mazao ya biashara jitihada zitafanyika ili kuongeza uwezo wa kusindika pamba, korosho, kahawa, pareto na zabibu.

**Huduma za Ugani**

41. Mheshimiwa Spika, tunapenda kuzihimiza Serikali za Mitaa kuhakikisha kwamba zinaandaa mipango mizuri ya kuwatumia maafisa ugani na kuwawezesha kufanya kazi zao kikamilifu na kwa ufanisi. Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Serikali za Mitaa, itahakikisha kwamba maafisa kilimo wanapata mafunzo ya kutosha, wanapata matokeo ya utafiti na kuyafikisha kwa wakulima na wanapatiwa vitendea kazi kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu. Huduma za ugani kwa wakulima zitaendelea kuimarishwa, kwa kutoa mafunzo kwa vikundi vya ushirikishwaji ambavyo vitaanzishwa vijijini.

42. Muundo wa usimamizi wa shughuli za Kilimo katika Serikali za Mitaa na Mikoa utaangaliwa upya ili kuuimarisha na kuhakikisha kwamba huduma za ugani zinamfikia mkulima ipasavyo, kwamba maelekezo ya sera na utaalam yanawafikia maafisa ugani na yanatekelezwa kwa wakati na kwamba maafisa ugani wanatoa taarifa juu ya shughuli zao kwa vipindi vilivyowekwa. **Haya yakitekelezwa, mpango wa kuwahamishia maafisa ugani kwenye Serikali za Mitaa utakuwa na manufaa yaliyokusudiwa.**

**Bodi ya Mazao Mchanganyiko**

43. Mheshimiwa Spika, mazao yote ya chakula, mbegu za mafuta, viungo *(spices)*, maua, matunda na mboga hayana chombo cha kuyaendeleza na kudhibiti mwenendo wa uzalishaji na uuzaji wake. Hali hii imetokana na kufa kwa GAPEX iliyokuwa ikisimamia mbegu za mafuta na mazao mengine yasiyo asilia. Aidha, Shirika la Kilimo na Chakula *(NAFCO)*, ambalo limekuwa likiendesha mashamba makubwa ya nafaka, hususan mpunga, ngano na mahindi, liko katika hali ngumu na linabinafsishwa na Shirika la Usagishaji la Taifa nalo linabinafsishwa. Katika mwaka wa 2001/2002 Wizara itaanzisha Bodi itakayounganisha mazao ambayo yalikuwa yakishughulikiwa na mashirika hayo matatu.

**Mbolea na Madawa ya Kilimo**

44. Wizara itaweka utaratibu wa kuwatambua waagizaji wa mbolea na madawa ya kilimo na kuwasajili, kubaini mipango yao ya kuingiza mbolea nchini, wanakopata mbolea na kuthibitisha ubora wa mbolea hiyo. Kuweka utaratibu wa kushauriana mara kwa mara na waingizaji na wasambazaji wa mbolea kwa lengo la kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi na kufikisha mbolea kwa wananchi kwa wakati na kwa gharama nafuu. Kituo cha Utafiti cha Mlingano kitaimarishwa ili kiweze kuthibitisha ubora wa mbolea na kuzuia uingizaji wa mbolea isiyokuwa na sifa zitakiwazo. Aidha, taasisi ya TPRI itaendelea na udhibiti wa uingizaji wa madawa ya mimea *(Pesticides)* ili kuhakiki ubora wake.

**Mbegu**

45. Ili kuimarisha mfumo wa uzalishaji mbegu, **mashamba ya mbegu za msingi ya Serikali** (*foundation seed farms*) **hayatabinafsishwa** na badala yake **yatasimamiwa na chombo maalum kitakachoundwa. Wizara** ya Kilimo na Chakula **inaandaa mfumo mpya wa kusimamia uzalishaji wa mbegu mama za watafiti (*breeders' seed*), mbegu za msingi** (*foundation seed*) **na mbegu zilizothibitishwa** (*certified seed*). Aidha, Wizara ya Kilimo na Chakula **itaendelea kutoa utaalam kwa vikundi vya wakulima wadogo kuzalisha mbegu zisizokuwa chotara** ili waweze kuwauzia wakulima wenzao kwa bei nafuu.

***Mradi wa Kuongeza Rutuba Kwenye Udongo na Tija Katika Kilimo (Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project – SOFRAIP)***

46. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002, Wizara itaanza utekelezaji wa Mradi wa Kuongeza Rutuba Kwenye Udongo na Tija katika Kilimo *(Soil Fertility Recapitalization and Agricultural Intensification Project – SOFRAIP).* Lengo kuu la mradi ni kuongeza tija katika kilimo na kuwaongezea wakulima wadogo mapato. Mradi huo utatekelezwa nchi nzima. Katika mwaka wa 2001/2002 mradi utaanza kutekelezwa katika wilaya 16 zitakazoteuliwa kwa utaratibu utakaowekwa. Kazi zitakazotekelezwa chini ya mradi huu ni pamoja na kuongeza matumizi sahihi ya zana na pembejeo za kilimo (mbolea, mbegu, madawa); kuboresha utaratibu wa kuagiza pembejeo kwa lengo la kupunguza bei, kukarabati maabara nne za kupima udongo *(Mlingano, Selian, Ukiriguru na Uyole)*; kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalam na kueneza mbinu bora za kutunza na kuhifadhi udongo. Aidha, **mradi utaanzisha utaratibu wa mikopo kwa wakulima** utakaotumia vocha kupitia kwenye Vyama vyao vya Ushirika au vya Kuweka na Kukopa. Kwa utaratibu huu, mkulima atatakiwa kulipa nusu ya gharama za pembejeo na nusu iliyobakia italipwa na chama chake. Utaratibu huu unasisitiza umuhimu wa wakopaji kulipa madeni yao bila kukosa. Mradi huo utaongeza uzalishaji wa mahindi kwa asilimia 60 kutoka tani 2,600,000 mwaka wa 2000/2001 hadi tani 5,000,000 mwaka wa 2005/2006 na **hivyo kuwezesha nchi yetu kujitosheleza kwa Chakula.**

**Kuhimiza Uzalishaji wa Mazao Kufuatana na Kanda za Kilimo *(Agro-ecological zones)***

47. Mheshimiwa Spika, Wizara imekwishaainisha mazao yanayofaa kwa kila kanda *(Kiambatanisho Na. 6)*. Serikali za Mitaa zitashauriwa kusimamia wakulima kulima mazao yanayostawi katika maeneo yao na kutunga sheria ndogo kwa ajili hiyo. Kwa maeneo kame, kipaumbele kitawekwa kwenye kilimo cha mazao yanayostahimili ukame kama vile muhogo, viazi vitamu, mtama na uwele.

**Huduma za Utafiti wa Kilimo**

48. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 msukumo utawekwa katika maeneo ya utafiti yafuatayo:

(i) Utafiti wa mazao kuhusu aina bora za mbegu zinazostahimili ukame, magonjwa, wadudu waharibifu na zenye mavuno mengi. Lengo litakuwa kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija na faida kwa wakulima. Utafiti huu utafanyika katika mashamba ya wakulima wenyewe. Aidha, utaalam wa kisasa wa kupata mbegu bora za mimea ujulikanao kama *"Biotechnology"* utaanzishwa na kuimarishwa katika vituo vya Utafiti vya Mikocheni, Mlingano, Tengeru, Uyole na Lyamungo;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji mashambani katika vituo vya Ilonga, Uyole, Selian, Tumbi, Mlingano, Naliendele na Ukiriguru kwa lengo la kufupisha muda wa upatikanaji wa mbegu bora vituoni kwa kuwezesha kupanda mara mbili kwa mwaka;

(iii) Utafiti juu ya matumizi bora ya viuwadudu na mbolea kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji na kumwezesha mkulima kupata faida kubwa zaidi;

(iv) Kuzalisha na kusambaza mbegu bora mpya za kahawa zinazovumilia ugonjwa wa Cheribuni *(Coffee Berry Disease CBD)*, na kutu ya majani *(Leaf rust); na*

(v) Kukamilisha uzalishaji *(multiplication)* wa mbegu ya pamba aina ya **UK 92,** na kuisambaza kwa ajili ya kulimwa katika kanda **yote** ya Magharibi.

**Kilimo cha Umwagiliaji Maji**

49. Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2001/2002 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 535.0 fedha za hapa na shilingi bilioni 10.06 fedha za nje kwa ajili ya kujenga na kukarabati miradi ya umwagiliaji maji mashambani ifuatayo: Mradi wa Usimamizi wa Mabonde ya Mito Rufiji na Pangani na Uboreshaji wa Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani kwa Wakulima Wadogo (*Rufiji and Pangani River Basins Management and Smallholder Irrigation Improvement Project)*, Programu ya Kusaidia Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Programme Support- ASPS*), Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (*Participatory Irrigation Development Programme-PIDP*), na Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji maji wa Mwega (Morogoro). *(Viambatanisho Na. 5 na Na. 7).* Aidha, kwa msaada wa Serikali ya Japan, Serikali inaandaa mpango kabambe wa kitaifa wa umwagiliaji maji mashambani *(National Irrigation Master Plan)*, utakaotekelezwa katika mikoa yote ishirini.

**Hifadhi na Usalama wa Chakula**

50. Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Hifadhi ya Chakula cha Taifa *(Strategic Grain Reserve SGR)* kitanunua tani 20,000 za mahindi kutokana na shilingi 1,432,650,000 zilizotengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa

2001/2002 na shilingi 1,000,000,000 kutoka mauzo ya mahindi ya akiba, hivyo kufikia jumla ya tani 65,000 za mahindi mwaka wa 2001/2002.

**Kujitosheleza kwa Chakula**

51. Mheshimiwa Spika, kujitosheleza kwa chakula ni lengo la msingi la Serikali. Katika mwaka wa 2001/2002, Wizara ya Kilimo na Chakula, kwa kushirikiana na washikadau wengine wa sekta ya Kilimo, itaanza kutekeleza mipango ya makusudi ya kuiwezesha nchi kujitosheleza kwa chakula kwa utaratibu endelevu. Hatua zifuatazo zitachukuliwa:

**Uzalishaji wa Mpunga**

52. Mahitaji ya mchele kitaifa katika mwaka wa 2001/2002 ni tani 556,320 *(au tani 855,877 za mpunga).* Uzalishaji katika msimu wa 2000/2001 ulikuwa ni tani 790,014 za mpunga sawa na tani 513,509 za mchele. Kwa hiyo kutakuwa na upungufu wa tani 42,810 za mchele ambao utazibwa na uagizaji wa mchele kutoka nje pamoja na misaada ya chakula kutoka kwa wahisani, hususan Serikali ya Japan. Mikakati ya kujitosheleza kwa mahitaji ya mchele ni pamoja na kubinafsisha mashamba ya mpunga ya NAFCO yenye uwezo wa kuzalisha tani 100,900 za mpunga kwa mwaka, kufufua miradi ya umwagiliaji iliyojengwa miaka iliyopita inayokisiwa kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 66,045 za mpunga, kupanua baadhi ya miradi iliyoko na kukamilisha ile inayoendelea kujengwa na kadri uwezo wa Serikali utakavyoruhusu, kuanzisha miradi mipya ya kilimo cha mpunga. Kuandaliwa kwa mpango Kabambe wa Umwagiliaji Maji Mashambani katika miaka miwili na nusu ijayo kutawezesha kuandaliwa kwa mipango mipya ya umwagiliaji. Nchi yetu ina uwezo mkubwa wa kuwa muuzaji mkubwa wa mchele nje ya nchi.

**Sukari**

53. Inakisiwa kwamba mahitaji ya nchi ya sukari ni zaidi ya tani 300,000 kwa mwaka. Baada ya kubinafsishwa kwa mashamba makubwa ya miwa ya Kilombero, Mtibwa na TPC., uzalishaji wa sukari umeongezeka kutoka tani 113,622 za sukari mwaka wa 1998/1999 hadi tani 135,500 mwaka wa 2001. Uzalishaji wa sukari kwenye mashamba hayo unatarajiwa kuendelea kuongezeka hadi kufikia tani 273,000 mwaka wa 2005. Katika mwaka wa 2001/2002 hatua zitachukuliwa kubinafsisha shamba la miwa la Kagera lenye uwezo wa kuzalisha tani 56,000 za sukari na baadaye kuanzisha mashamba mapya Ikongo mkoani Mara na Mahurunga mkoani Mtwara. Katika miaka ijayo itabidi kuanzisha mashamba mapya ya miwa na kuongeza juhudi za kuanzisha mashamba ya miwa ya wananchi na viwanda vidogo vya kusindika miwa. Aidha, viwanda vya sukari vinahimizwa kuzalisha sukari ya kutumika viwandani ili taifa liache kuagiza sukari hiyo kutoka nje.

**Uzalishaji wa Mahindi**

54. Mahindi ndiyo chakula kikuu cha Watanzania wengi na kwa hali hiyo, kujitosheleza kwa chakula kunategemea sana kujitosheleza kwa mahitaji ya mahindi. Kilimo cha mahindi kinategemea mvua. Hatua zitachukuliwa kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo, kusambazwa kwa mbegu mpya zinazostawi kwenye maeneo mengi ya nchi na zinazotoa mazao mengi na kuimarisha huduma za ugani ambazo kwa pamoja, zitawawezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa mahindi kukidhi mahitaji ya nchi na kuzalisha ziada ya kuuza nje ya nchi. Kuanzia msimu wa 2001/2002 Serikali itaanza kuzalisha mbegu ya msingi ya aina mpya ya mahindi yenye *'protein'* nyingi na, kwa hiyo, yenye uwezo wa kudhibiti utapiamlo.

**Mazao Yasiyo Asili**

55. Mazao ya chakula yasiyo asili yana nafasi kubwa katika kuinua ubora wa chakula na mengi ya mazao hayo yana masoko yenye bei nzuri na ushindani mdogo ndani na nje ya nchi. Tunaishauri mikoa irekebishe dosari za uzalishaji zilizoko na tushirikiane kukuza uzalishaji wa mazao haya na kuyatafutia masoko.

**Kupambana na Janga la UKIMWI katika Sekta ya Kilimo**

56. Mheshimiwa Spika, UKIMWI unapunguza nguvukazi ya kilimo na kuathiri uzalishaji. Katika mwaka 2001/2002, Wizara itaendelea kuwaelimisha wakulima na wafanyakazi namna ya kupambana na janga hili.

## V. HITIMISHO

57. Mheshimiwa Spika, maendeleo ya Kilimo yanategemea washikadau wa Sekta ya Kilimo, wengi wakiwa nje ya Wizara ya Kilimo na Chakula. Tunawahimiza washikadau wajitahidi kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Wakulima wajitahidi kupanua mashamba yao na wayalime kwa mbinu za kisasa, wapambane na wadudu na wanyama waharibifu na watunze mazao dhidi ya wadudu waharibifu. Serikali itajitahidi kuweka mazingira yatakayowezesha kupatikana kwa mahitaji ya kilimo, yakiwa ni pamoja na utaalam wa kilimo cha kisasa, kuboresha miundo mbinu, hususan barabara na kuwasaidia wakulima kupata masoko ya uhakika na yenye bei nzuri. Aidha, Serikali itachukua hatua za kudhibiti ukiritimba miongoni mwa wanunuzi wa mazao na kumhakikishia mkulima soko la haki. Kilimo kitaendelea kuongozwa na sekta binafsi na tunaitaka sekta hiyo iendeshe shughuli zake kwa ufanisi, uwazi na kwa viwango vinavyotakiwa na kwa maslahi ya wakulima na taifa kwa ujumla.

58. Baada ya kusema yote hayo, mkulima anahitaji kujiunga na Vyama vya Ushirika vitakavyomwongezea nguvu, kumlinda dhidi ya ushindani usiokuwa wa haki, kumtafutia mahitaji muhimu ya kilimo, kusindika mazao yake ili kuyaongezea thamani na kutafuta masoko ndani na nje ya nchi.

## VI. SHUKRANI

59. Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii kuwashukuru tena, Waheshimiwa Wabunge, hususan Wajumbe wa Kamati ya Kisekta ya Uzalishaji Mali inayoongozwa na Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa kuchambua makisio haya na kuyapitisha.

60. Mheshimiwa Spika, napenda kuzishukuru nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa yafuatayo ambayo yanaendelea kusaidia Wizara ya Kilimo na Chakula katika juhudi za kuleta mageuzi katika Sekta ya Kilimo. Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Israeli, Italia, Japan, Korea Kaskazini, Korea Kusini, Marekani, Misri, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi na Sweden. Vile vile, Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo:- Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, EU, UNICEF, SADC, WFP, IFAD, CIMMYT, ICRAF, ICRISAT, ASARECA, IITA na Sasakawa Global 2000. Bado tunahitaji misaada yao ili tuweze kuendeleza kilimo.

61. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa wakulima wa Tanzania kwa kazi nzuri wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na ya biashara katika mazingira magumu ya ukosefu wa pembejeo muhimu, teknolojia ya kisasa na kilimo cha kutegemea mvua. Pia napenda kuwashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Profesa Pius P. Mbawala (Mb), Katibu Mkuu Ndugu Wilfred Ngirwa, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara ya Kilimo na Chakula kwa kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

62. Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Uchaguzi la Ubungo kwa kunichagua kuwa mbunge wao. Naahidi kushirikiana nao kwa dhati katika hatua za kuleta maendeleo endelevu kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

63. Mheshimiwa Spika, mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

## V. MAOMBI YA FEDHA 2001/2002

64. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo haya, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi 9,176,645,900 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi 15,957,400,000 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizi shilingi 1,421,000,000 ni fedha za hapa na shilingi 14,536,400,000 ni za nje.

**65. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja**.

**Jedwali Na.1: Hali ya Chakula 2000/2001**

| Mazao | Mahitaji (tani) | Uzalishaji (tani milioni) | Ziada/pungufu tani milioni |
|---|---|---|---|
| **Nafaka** | 4.788 | 3.370 | -1.418 |
| **Yasiyo nafaka** | 3.087 | 3.940 | +0.853 |
| **Jumla** | **7.875** | **7.310** | **-0.565** |

***Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula***

**Jedwali Na.2: Hali ya Chakula mwaka 2001/2002**

| Mazao | Mahitaji (tani milioni) | Uzalishaji (tani milioni) | Ziada/pungufu (tani milioni) |
|---|---|---|---|
| Nafaka | 4.948 | 4.125 | -0.823 |
| Yasiyo nafaka | 3.182 | 3.586 | +0.404 |
| **Jumla** | **8.131** | **7.712** | **-0.419** |

***Chanzo: Wizara ya Kilimo na Chakula***